# MABADILIKO YA KIMOFOFONEMIKI KATIKA MSAMIATI MKOPO WA KIKIPSIGIS

*Cherono Naomi J., Munyua J. G.,* na *Ogechi, N. O.*
*Chuo Kikuu cha Moi*
*Idara ya Kiswahili na Lugha nyingine za Kiafrika*
*2019, Moi University Press*

**Ikisiri**

Kila lugha ni mfumo huru unaojitosheleza kisarufi. Ingawa hivyo, wasemaji wa lugha tofauti wanapotagusana kimawasiliano, lugha zao huweza kuathiriana kisarufi, na athari mojawapo huwa ni ukopaji wa msamiati. Ni kutokana na hali hii ambapo utafiti huu ulichunguza kanuni zinazofuatwa katika uingizwaji wa msamiati mkopo wa Kiswahili na Kiingereza katika Kikipsigis. Makala hii ilichunguza mabadiliko ya kimofofonemiki yanayotokea katika msamiati mkopo unapoingizwa katika mfumo wa Kikipsigis. Vilevile, sababu za ukopaji zilibainishwa. Data ya utafiti iliteuliwa kimakusudi. Utafiti ulitambua kuwa Kikipsigis hufupisha irabu ndefu katika msamiati mkopo. Vilevile, irabu unganifu husahilishwa ili zikubalike katika Kikipsigis. Kimsingi tulitambua kuwa Kikipsigis hutohoa irabu ngeni kwa kutumia irabu asili zinazokaribiana kimatamshi. Ilibainika pia kwamba Kikipsigis hakiruhusu mfuatano wa konsonanti mwanzoni mwa neno. Kwa hivyo, Kikipsigis hutohoa msamiati wa aina hii kwa kuchopeka irabu. Katika kuchunguza vichocheo vya ukopaji, makala hii ilibainisha kwamba Kikipsigis hukopa msamiati ili kurejelea dhana ngeni isiyokuwepo katika utamaduni wake. Hata hivyo, uchanganuzi ulionyesha kuwa Kikipsigis wakati mwingine hukopa msamiati hata kama kina msamiati asilia kwa sababu ya ubadilishaji msimbo, msamiati mkopo ni sahili na rahisi kutamkwa ukilinganishwa na kisawe chake cha Kikipsigis.

**Maneno Muhimu:** *Msamiati Mkopo***,** *Utohozi, Mabadiliko ya Kimofofonemiki*

## Utangulizi

Kikipsigis kimejumuisha msamiati mkopo katika dafina yake ya msamiati. Msamiati hiyo mkopo imetoka katika lugha mbalimbali ikiwemo Kiswahili na Kiingereza. Misamiati hiyo haitumiki tu katika lugha semwa bali pia katika maandishi. Utafiti huu ulichunguza namna ambavyo Kikipsigis hutohoa msamiati unaokopwa kutoka Kiswahili na Kiingereza ili ikubalike katika mfumo wake wa kifonolojia na kimofolojia. Utohozi hufanya msamiati mkopo kuchukua muundo wa msamiati katika Kikipsigis. Kwa hivyo tulijiuliza je utohozi unaathiri vipi irabu na konsonanti za lugha husika? Tulichunguza mabadiliko haya kwa kuzingatia utohozi wa fonimu ambapo tulianza kwa kuchunguza utohozi wa irabu na kisha utohozi wa konsonanti.

Lugha za Kiafrika zimegawika katika makundi manne makuu: Nilo-Sahara, Niger-Congo, Afro-Asiatic na Khoisan. Kikipsigis ni mojawapo wa lahaja za Kikalenjin zinazopatikana katika kikundi cha Nilo-Sahara. Kikalenjin ni lugha ya kinailotiki inayozungumzwa nchini Kenya, Uganda Mashariki (Sebei) na Kaskazini mwa Tanzania (Dagota) (Sang & Jerono 2012). Kikalenjin kina lahaja nane ambazo ni Kipsigis, Nandi, Tugen, Keiyo, Marakwet, Sabaot, Pokot, Terik, Seng'wer na Okiek (Seroney,2009). Kati ya lahaja hizi, Kipsigis ndiyo iliyo na wasemaji wengi (Sambu, 2007). Wasemaji wa lugha hii walianza kutagusana na waingereza katika karne

ya 18. Kufikia karne ya 19 mitagusano yao iliendelezwa na majilio ya wamishenari waliofika Afrika kueneza dini ya kikristo na pia walowezi kutoka Uingereza ambao walizumgumza Kiingereza na baadaye kujifunza lugha za wenyeji ikiwemo Kiswahili (Sang & Jerono, 2012). Kwa hivyo, wamishenari na walowezi walitagusana na Wakipsigis kupitia matumizi ya Kiswahili.

**Dhana ya ukopaji**

Myers-Scotton (2002) anaeleza kuwa mojawapo ya matokeo ya ujozi-lugha ni ukuzaji wa elementi za kileksia baina ya lugha zinazohusika ambapo lugha iliyo na hadhi ya chini hukopa msamiati kutoka lugha iliyo na hadhi ya juu. Anazidi kueleza kuwa kuna aina mbili za ukopaji: ukopaji wa kiutamaduni na ukopaji wa kimtindo. Ukopaji wa kiutamaduni unarejelea ukopaji wa msamiati wa kurejelea dhana au vitu ambavyo ni vya kigeni katika utamaduni wa lugha husika. Hapa, msamiati-mkopo huweza kubeba sifa za kifonolojia kutoka lugha changizi hadi lugha pokezi. Kwa upande mwingine, ukopaji wa kimtindo hurejelea ukopaji wa msamiati unaowakilisha dhana zilizopo tayari katika lugha pokezi. Msamiati wa aina hii huingizwa sana katika lugha husika kwa sababu ya ubadilishaji msimbo.

Iribemwangi na Mukhwana (2011) wanaeleza kuwa ukopaji wa maneno huenda sambamba na urekebishaji wa neno ili lifuate kanuni za kifonolojia za lugha pokezi. Urekebishaji huu ndio utohozi na hufanya neno likubalike katika lugha hiyo pokezi. Hii ni kusema kuwa lugha hutumia ukopaji katika kujiongezea msamiati haja inapotokea. Yule (2006) anaelea kuwa njia kuu ya upanuzi wa msamiati katika lugha ni mbinu ya ukopaji wa maneno ambapo neno fulani huchukuliwa kutoka lugha changizi na kuingizwa katika lugha pokezi. Upanuzi wa misamiati husababisha mabadiliko katika lugha husika. Lugha hupanua msamiati wake ili kuweza kurejelea dhana geni na kuwezesha mahitaji ya kimawasiliano katika jamii. Bright (1997) katika Coulmas (1997) anaeleza kuwa lugha hubadilika mara kwa mara katika muundo wake (fonolojia, sarufi, semantiki na misamiati).Lugha hukopa msamiati kutoka lugha nyingine kutokana na sababu za kiisimu-jamii. Whitefield (1970) anaeleza kuwa neno halikopwi tu kwa sababu dhana ambayo neno hilo linarejelea haipatikani katika lugha pokezi, ila watu hukopa kwa kuwa neno hilo ni la kigeni na kuonekana kuwa zuri zaidi kuliko lile asilia. Vilevile ukopaji husababishwa na maendeleo ya kisayansi na kiteknolojia na hata kuibuka kwa dhana geni katika nchi. Isitoshe, ubadilishaji msimbo katika mazingira ya mtagusano-lugha huweza kuleta ukopaji kati ya lugha solo na lugha bebwa (Myers-Scotton 1997). Utafiti wetu ulizigatia maelezo ya wataalamu hawa katika kuchunguza sababu zinazoifanya lugha ya Kikipsigis kukopa msamiati kutoka lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

**Ukopaji na ujozi lugha**

McMahon (1994) anaeleza kuwa kwa kiwango fulani ukopaji hutegemea ujozi lugha. Anafafanua kuwa mchakato wa lugha moja kukopa msamiati kutoka lugha nyingine hutegemea ujuzi alionao mtu huyo kuhusu lugha zote husika (lugha changizi na lugha pokezi). Nao LaCharite na Paradis (2000) wanaeleza kuwa wakopaji wa msamiati wa kileksia ni wana-ujozi lugha na wanapaswa kufahamu fonolojia ya misimbo yote miwili yanayohusika katika ukopaji; yaani fonolojia ya lugha changizi na lugha pokezi. Kutokana na ufahamu huu basi wao huweza kuhamisha sauti kutoka lugha moja, lugha changizi hadi lugha nyingine, lugha pokezi. Wanaisimu hawa wanazidi kufafanua kuwa baada ya wanaujozi lugha kutohoa msamiati katika lugha pokezi, basi wanajamii wengine huutumia msamiati huo uliotoholewa. Msamiati huo huwa

umekubaliwa na jamii ya wanaujozi lugha. Wanatoa mfano wa fonimu /x/ ambao ni sauti ya Kiarabu lakini imekopwa katika Fula na wanaujozi lugha walio na ujuzi wa Fula na Kiarabu waliosoma katika shule za Koran. Baada ya wanaujozi lugha hao kukopa fonimu hii inakubalika katika jamii na kutumiwa na wanajamii wengine. Utafiti wetu vilevile ulibainisha kuwa katika jamii ya Wakipsigis wapo wanaumoja lugha wanaotumia msamiati mkopo bila hata kufahamu ulitoka katika lugha gani ila kwa sababu umekubalika na kutumika katika jamii nao pia wameutumia namna unavyotumika na wanajamii wengine.

**Ukopaji na ubadilishaji msimbo**

Myers-Scotton (1993) anaeleza kwamba ukopaji huhusisha matumizi ya msamiati mkopo ambao unasambaa na kutumika katika jumuiya lugha na huwa umekubalika katika jamii husika. Nao Paradis na LaCharite (1997) wanaeleza kuwa katika ukopaji, msamiati mkopo huingizwa katika lugha solo na kutoholewa kufuata mfumo wa lugha hiyo kimofolojia, kifonolojia na hata kisintaksia. Ubadilishaji msimbo kwa upande mwingine huhusisha matumizi ya maneno ya kigeni ambayo hayatoholewi kifonolojia au kimofolojia katika lugha solo. Myers-Scotton (1992) anafafanua kwamba tofauti nyingine kati ya ubadilishaji msimbo na ukopaji upo kwenye mtindo wa urudufu wa msamiati mkopo na uwezo wa kutabiri utohozi wake. Kwamba ukopaji katika lugha solo hutokea mara kwa mara na kuna uwezekano wa kutabiri mchakato wake wa kiutohozi katika lugha solo.  Hata hivyo katika ubadilishaji msimbo maneno yanayotumika hutokea mara chache na hayatabiriki. Vilevile msamiati mkopo hutumika sana katika maneno ambayo ni ya kigeni katika jumuiya lugha fulani.

Naye Muysken (1995) anaeleza kuwa ubadilishaji msimbo ni matumizi ya lugha mbili katika kishazi au tamko moja. Anafafanua kuwa ubadilishaji msimbo hutofautiana na dhana ya ukopaji kileksia kwa sababu katika ukopaji elementi za kileksia kutoka lugha moja huingizwa katika leksia ya lugha nyingine ambayo ni pokezi. Ubadilishaji msimbo kwa upande wake ni zao la mazungumzo kati ya wanaujozi lugha. Asher & Simpson (1994) nao wanaeleza kuwa dhana ya ukopaji hurejelea maneno ya kigeni ambayo huingizwa katika leksia ya lugha pokezi lhali ubadilishaji msimbo huhusisha matumizi ya maneno ya lugha nyingine katika lugha pokezi lakini maneno hayo huwa hayaingizwi katika leksia ya lugha hiyo pokezi. Hatua hii ya kutofautisha baina ya ubadilishaji msimbo na ukopaji katika utafiti huu ni muhimu kwa kuwa tuliangazia msamiati mkopo na hivyo basi kuweka tofauti ya dhana hizi wazi ulituwezesha kukusanya data iliyotoholewa kikamilifu katika lugha pokezi ambayo ni Kikipsigis.

## Utohozi wa Irabu za Kiingereza

Kiingereza kina irabu saba fupi [I, ʊ, Λ, æ, ɒ, e, ə] irabu tano ndefu [iː, ʒː, ɑː, ɔː, uː] na irabu unganifu nane. Kikipsigis kwa upande mwingine kina irabu kumi. Hali hii inabainisha kuwa kuna tofauti kati ya irabu za lugha hizi mbili ambapo kuna irabu zilizopo katika Kiingereza (kama vile irabu unganifu) lakini hazipo katika Kikipsigis. Kwa hivyo, utafiti huu ulichunguza namna irabu hizi za Kiingereza hutoholewa katika Kikipsigis na kile kinachoamua uteuzi wa irabu fulani kujaza pengo la irabu isiyokuwepo katika Kikipsigis. Ilibanika kwamba utohozi wa fonimu irabu hutokea kupitia michakato ifuatayo:

**Ufupishaji wa irabu ndefu**

Irabu ndefu hurejelea irabu zilizo na urefu kimatamshi zikilinganishwa na irabu fupi katika muktadha unaofanana (Roach, 2000). Urefu wa irabu hutofautiana kulingana na muktadha wa

matumizi kwa mfano aina ya sauti inayofuata irabu husika na vilevile kuwepo au kutokuwepo kwa mkazo. Ilibainika katika utafiti huu kwamba irabu ndefu katika msamiati wa Kiingereza hufupishwa unapoingizwa katika Kikipsigis. Kwa mfano irabu ndefu /ɜː/ hufupishwa kuwa irabu fupi /a/ au /ɔ/. Hali hii hutokana na kutokuwepo kwa irabu ndefu /ɜː/ katika Kikipsigis. Mifano ifuatayo inathibitisha utohozi huu:

**/ɜː/ → /a/**

| **Kiingereza** | | | **Kikipsigis** | |
|---|---|---|---|---|
| [nɜːsəri] | | → | [nasarɛt] | 'nursery' |
| | ɜː | → | A | |
| [θɜːməs] | | → | [tamɔsit] | 'thermos' |
| | ɜː | → | A | |

**Usahilishaji wa irabu unganifu**

Irabu unganifu hurejelea irabu mbili zinazotamkwa kwa kuunganishwa (TUKI 1990). Katika Kiingereza kuna irabu unganifu nane. Irabu hizi huingizwa katika Kikipsigis kwa kusahilishwa ili zikubalike katika mfumo wa kifonolojia wa Kikipsigis:

**/eI/ → /ɛ/**

| **Kingereza** | | | **Kikipsigis** | |
|---|---|---|---|---|
| [fr**eI**m] | | → | [prɛmit] | 'frame' |
| | **eI** | → | **E** | |
| [r**eI**diəʊ] | | → | [rɛtiɔ] | 'radio' |
| | **eI** | → | **E** | |
| | əʊ | → | ɔ | |

Katika mifano hii irabu unganifu /eI/ imesahilishwa kuwa irabu /ɛ/ katika Kikipsigis kupitia mchakato wa kusahilisha irabu unganifu kwa kuwa Kikipsigis hakina irabu unganifu. Katika mifano hii, tulibainisha kuwa utohozi wa irabu unganifu /**əʊ/** kuwa /ɔ/ huenda unatokana na orthografia wa msamiati mkopo katika Kiingereza. Kwa hivyo, maneno haya yametoholewa kulingana na fonolojia wa maneno haya katika Kiingereza. Kwa kuwa Kikipsigis hakina konsonanti /h/, basi inadondoshwa na ndio maana neno (hotel) likakopwa kuwa [oteliit].

**Uyeyushaji**

Uyeyushaji hurejelea mchakato wa kuundwa kwa kiyeyusho /j/ ama /w/ katika neno. Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa msamiati mkopo kutoka Kiingereza ulio na irabu tatu-unganifu hutoholewa kwa kuundwa kwa kiyeyusho kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

**/aIə/ → /aja/**

| **Kiingereza** | | **Kikipsigis** | |
|---|---|---|---|
| [daIəri] | → | [tajari] | 'diary' |
| [aIə] | → | [aja] | |
| [kwaIə] | → | [kwaja] | 'choir' |
| [aIə] | → | [aja] | |

Mifano hii inabainisha kuwa irabu tatu-unganifu [aIə] inatoholewa kupitia kuundwa kwa kiyeyusho kati ya irabu husika [aja]. Katika mifano hii, tuligundua vilevile kwamba kunatokea uimarikaji wa irabu ambapo irabu /I/ ambayo ni mojawapo wa irabu tatu-unganifu,

imebadilishwa kuwa nusuirabu /j/. Fonimu za irabu huimarika wakati ambapo irabu husika hubadilika na kuwa nusu irabu. Kwa kuwa irabu /I/ hutumia nguvu hafifu wakati wa kutamka, inapobadilishwa kuwa /j/ inayotumia nguvu nyingi katika utamkaji wake, basi tunasema kwamba irabu /I/ imeimarika.

**Muungano wa irabu**

Muungano wa irabu ni mchakato unaotokea wakati ambapo irabu zinaathiriana na irabu fulani kupoteza sifa zake zote bainifu kwa irabu jirani au pengine irabu zote mbili kuungana na kuzua alofoni mpya ya fonimu inayohusika (Habwe na Karanja, 2004). Katika utafiti huu, tulibainisha kwamba irabu tatu-unganifu hutoholewa kupitia kwa kuunganishwa kwa irabu mbili kati ya hizo tatu-unganifu kama inavyobainika katika mifano ifuatayo:

**/Iəʊ/ → /iɔ/**

Aina hii ya irabu tatu-unganifu hutokea mwishoni mwa neno jinsi ilivyo katika msamiati radio. Irabu hizi unganifu [**Iəʊ],** hutoholewa kuwa **[io]** kupitia kuunganishwa kwa irabu mbili za mwisho, yaani [Iəʊ] kuwa [o] ili kuunda irabu [io] inayokubalika katika Kikipsigis kama ilivyo katika mfano ufuatao:

| Kiingereza | | Kikipsigis | |
|---|---|---|---|
| [reIdiəʊ] | → | [rɛtiɔ] | ‘radio’ |
| [Iəʊ] | → | [iɔ] | |

Kwa hivyo, hapa tunaona kwamba msamiati mkopo ulio na irabu tatu-unganifu hutoholewa kupitia ama uyeyushaji au muungano wa irabu.

## Utohozi wa irabu za Kiswahili

Kiswahili kina jumla ya irabu tano ambazo ni /a/, /ɛ/, /i/, /ɔ/ na /u/ ilhali Kikipsigis kina irabu kumi. Irabu hizi tano za Kiswahili zinapatikana katika Kikipsigis. Utafiti ulibainisha mabadiliko yafuatayo katika utohozi wa irabu za Kiswahili:

**Uchopezi wa irabu**

Uchopezi ni utaratibu wa kifonolojia unaotumika kudhibiti mpangilio halali wa sauti katika lugha yoyote iwayo kupitia uingizaji wa irabu, konsonanti au kiyeyusho katika msamiati husika (Kadurenge 1995). Kwa hivyo katika mchakato huu, irabu huingizwa katika sehemu fulani ya neno linalokopwa ili kulifanya neno hilo kufuata mfumo wa kifonolojia wa lugha husika. Hali hii hutokea katika Kikipsigis jinsi inavyobainika katika mifano ifuatayo:

**Uchopezi wa irabu kati ya konsonanti mbili au zaidi zinazofuatana**

Katika Kikipsigis, uchopekaji wa irabu hutokea katika msamiati mkopo ulio na konsonanti mbili au zaidi zinazofuatana mwanzoni mwa neno k.v.

| Kiswahili | Kikipsigis |
|---|---|
| [mcɛlɛ] | [m**u**cɛlɛk] |
| [mkatɛ] | [m**a**gatiat] |
| [mkɔra] | [m**a**gɔrajat] |
| [mʃahara] | [m**u**sjara] |
| [stima] | [s**i**timɛt] |

Katika mifano hii, tunaona kuwa uchopezi wa irabu huathiri maneno yanayoanzia kwa nazali /m/ na kufuatwa na konsonanti nyingine, kwa hivyo irabu huchopekwa ili kuruhusu msamiati mkopo kufuata muundo wa maneno katika Kikipsigis.

**Uchopezi wa irabu mwanzoni mwa msamiati**

Katika kutohoa msamiati wa Kiswahili unaonza kwa fonimu /$^{n}$g/ na /$^{n}$d/, Kikipsigis huchopeka irabu /i/ mwanzoni, yaani kabla ya fonimu hizo. Kwa mfano;

| **Kiswahili** | **Kikipsigis** |
|---|---|
| Ndizi | **i**ndisiɔt |
| Ndɛgɛ | **I**ndɛgɛit |
| Ngazi | **I**ngasit |
| nguɔ | **i**ngɔriɛt |

Ilibainika vile vile kwamba msamiati unaoanza kwa konsonanti /m/ na kufuatwa na konsonanti /p/ kama vile neno mpaka, unapokopwa katika Kikipsigis, irabu /i/ huchopekwa mwanzoni kama ilivyo katika mifano ifuatayo

| **Kiswahili** | **Kikipsigis** |
|---|---|
| Mpaka | **I**mbagait |
| Mpira | **I**mbirɛt |

Uchopezi wa aina hii hutokea kwa sababu Kikipsigis hakina mfuatano wa konsonanti /m/ na /p/. Kwa hivyo hubadilishwa kuwa /$^{m}$b/ na kutanguliwa na irabu /i/ inayochopekwa mwanzoni. Hali hii ipo katika msamiati asilia wa Kikipsigis kwa mfano: *imbaret* (shamba), *imborochot* (aina ya mboga ya kienyeji)

**Kuafikiana kwa irabu**

Mchakato huu hurejelewa pia kama tangamano la irabu. Kuafikiana kwa irabu ni ule utaratibu wa irabu fulani kukubali kuandamana katika mazingira maalum (Mgullu 1999). Tulibainisha kwamba utaratibu huu katika Kikipsigis husababishwa na irabu iliyo mwishoni mwa msamiati mkopo ambapo:

- Ikiwa irabu /a/ hutokea mwishoni mwa msamiati unaokopwa, basi utohozi wake huchukua silabi /ait/
- Ikiwa irabu /u/ ama /ɔ/ hutokea mwishoni mwa msamiati unaokopwa, basi utohozi wake huchukua silabi /oit/

Hali hizi zinadhihirika kupitia mifano inayofuata:
Msamiati mkopo ulio na irabu /a/

| **Kiswahili** | | **Kikipsigis** |
|---|---|---|
| Pich**a** | → | pich**ait** |
| Sa**a** | → | S**ait** |
| Cham**a** | → | cham**ait** |
| Chup**a** | → | chup**ait** |

Msamiati mkopo ulio na irabu /u/ ama /ɔ/

| Kiswahili | | Kikipsigis |
|---|---|---|
| Sim**u** | → | sim**ɔit** |
| kil**ɔ** | → | kil**ɔit** |
| Ping**u** | → | ping**ɔit** |

Hata hivyo, data ya utafiti huu ilibainisha kwamba kuna msamiati unaoishia kwa irabu hizi lakini hazifuati utaratibu huu wa tangamano la irabu kama vile:

| Kiswahili | | Kikipsigis |
|---|---|---|
| Nyany**a** | → | Nyany**at** |
| Chum**a** | → | chumɔ**yɔt** |
| Kitab**u** | → | Kitap**ut** |
| Elf**u** | → | **E**lip**ut** |
| Baf**u** | → | Pap**it** |

Hali hii ya msamiati kukosa kufuata utaratibu huu kwa maoni yetu pengine ni suala la ughairi ambapo umbo linakosa kufuata utaratibu unaotarajiwa wa kuafikiana kwa irabu.

Katika kuangazia mchakato huu wa kuafikiana kwa irabu, tuliweza kubainisha vilevile kwamba **mvutano wa irabu** hutokea katika baadhi ya msamiati kama inavyobainika ifuatavyo;

**Mvutano wa irabu**

Kama tulivyoeleza hapo juu, msamiati mkopo ulio na irabu /a/ mwishoni, hutoholewa kuwa na silabi /ait/, hata hivyo katika baadhi ya msamiati, kwa mfano msamiati 'kanisa' unapokopwa hubadilishwa kuwa 'kaniset' ilhali tungetaraji 'kanisait'. Hali hii hutokana na mchakato wa mvutano wa irabu. Irabu huvutana wakati ambapo irabu zimetokea kwa kufuatana ilhali irabu moja labda ni ya juu na nyingine ni ya chini (Mgullu 1999). Katika hali kama hiyo irabu hizo huvutana kiasi kwamba ile irabu ya juu inavutwa chini kidogo na ile ya chini inavutwa juu kidogo. Kwa hivyo, irabu inayotokea haitakuwa ya juu wala chini bali itakuwa ya kati. Katika Kikipsigis, mvutano wa irabu hutokea kati ya irabu /a/ ambayo ni ya chini na irabu /i/ ambayo ni ya juu. Mvutano huu hivyo basi huleta sauti moja tofauti ambayo ni irabu /ɛ/ iliyo kati ya irabu /a/ na /i/ kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

| Kiswahili | | Kikipsigis | |
|---|---|---|---|
| Daraja | → | tarac**a**+**i**t | → tarac**ɛ**t |
| Barua | → | baru**a** + **i**t | → baru**ɛ**t |
| Kanisa | → | kanis**a** + **i**t | → kanis**eɛ**t |
| kitanda | → | kitand**a** + **i**t | → kitand**ɛ**t |

**Udondoshaji wa irabu**

Udondoshaji ni hali ya kipashio cha neno; irabu, konsonanti au silabi kutoweka kabisa katika mazingira maalum ya kifonolojia au ya kimofofonemiki (Aswani 1995). Irabu hudondoshwa kwa sababu ya kuvunja mfuatano wa irabu katika msamiati ili kuudhibiti muundo wa silabi au ili kurahisisha matamshi na hivyo kuharakisha matamshi na mazungumzo. Hali hii hutokea Kikipsigis kinapotohoa msamiati kutoka Kiswahili ili kuruhusu msamiati huo kukubalika katika mfumo wa kifonolojia wa Kikipsigis. Data ya utafiti huu ilibainisha kuwa katika msamiati

mkopo ulio na irabu mbili zinazofuatana, Kikipsigis hudondoa irabu zote mbili au moja kati ya hizo irabu na kisha kuchopeka irabu nyingine. Kwa mfano;

| **Kiswahili** | **Kikipsigis** |
|---|---|
| b**ai**skɛli | pɔskilit |
| **[ai]→** | **[ɔ]** |
| [e]→ | [i] |
| serikali | Sergalit |
| [i]→ | [Ø] |

Katika [baiskeli] Kikipsigis hudondoa irabu zote mbili zinazofuatana, yaani /a/ na /i/ na kisha kuchopeka irabu /ɔ/, ilhali katika [saa], Kikipsigis hudondoa irabu moja /a/ na kuchopeka irabu /i/.

**Uyeyushaji**

Uyeyushaji hurejelea mabadiliko yanayokumba irabu ambapo irabu hubadilishwa kuwa nusu irabu.Mabadiliko haya hutokea katika mchakato wa utohozi ambapo irabu mbili tofauti zinapofuatana katika mazingira yasiyoruhusiwa katika Kikipsigis, hubadilishwa kuwa nusu irabu kama inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

| **Kiswahili** | | **Kikipsigis** |
|---|---|---|
| Mwalimu | mwalim**u** + **i**ɔt | →mwalimu**yot** |
| Fundi | pund**i** + **ɔ**t | → pundi**yot** |
| Mkora | magɔr**a** +**i**at | → magɔra**yat** |
| Mʃahara | mus**i** + **a**ra | → mus**ya**ra |
| Chuma | chumɔ + **iɔ**t | → chum**yɔt** |
| Dakika | tagig**a** + **ia**t | → tagiga**yat** |
| Malaika | malaig**a** + **ia**t | → malaiga**yat** |

Mifano hii imedhihirisha kwamba uyeyushaji hutokea katika baadhi ya msamiati mkopo kutoka Kiswahili ili kuepuka mfululizo wa irabu tatu. Hata hivyo ni vyema kutaja kwamba irabu hizi hubadilika kuwa viyeyusho bila kubadili maana ya msamiati husika.

## Utohozi wa konsonanti kutoka Kiingereza

Utafiti huu ulibainisha kuwa konsonanti katika msamiati mkopo wa Kiingereza unapoingizwa katika Kikipsigis hutoholewa kupitia michakato ifuatayo;

**Kuimarika kwa fonimu konsonanti**

Mgullu (1999) anaeleza kuwa utafiti wa muda mrefu uliofanywa na wanafonetiki katika maabara umethibitisha ya kuwa nguvu anazotumia mtu wakati anapotamka fonimu mbalimbali hutofautiana kutegemea aina ya sauti anayoitamka. Ziko fonimu ambazo huhitaji nguvu zaidi na zingine huhitaji nguvu kidogo. Vitamkwa visivyokuwa na mghuno hutumia nguvu zaidi kuliko vile vilivyo na mghuno. Kwa hivyo, sauti fulani huwa imeimarika kama inakuwa imebadilika kutoka kwenye aina ya sauti ambayo hutumia nguvu kidogo zaidi na kuwa sauti ambayo

inatumia nguvu nyingi zaidi. Hali hii hutokea katika Kikipsigis wakati ambapo kinakopa msamiati ulio na konsonanti zisizopatikana katika lugha hii. Konsonanti hizi ni kama vile /d/, /f/, /v/, /z/, /θ/, /δ/, /ɟ/ na /ɣ/. Sauti hizi hubadilishwa kwa zile sauti zilizopo katika Kikipsigis zinazokaribiana katika utamkaji. Kwa kufanya hivi, sauti hizo huweza kuimarika ama kudhoofika kwa kutegemea kiasi cha nguvu za misuli na msukumo wa mkondohewa katika utamkaji wa konsonanti hizo. Mifano ya mabadiliko yanayosababisha kuimarika kwa konsonanti ni zifuatazo:

**i. Vikwamizo (-ghuna) →vipasuo (-ghuna)**

Kulingana na orodha ya Mgullu, vikwamizo visivyo na mghuno viko chini katika ngazi ya tano ilhali vipasuo visivyo na mghuno viko juu katika ngazi ya kwanza. Basi kikwamizo kimebadilika kutoka ngazi ya chini inayotumia nguvu kidogo hadi ngazi ya juu inayotumia nguvu nyingi. Kwa hivyo, kubadilika kwa kikwamizo (-ghuna) hadi kwa kipasuo (-ghuna) ni tendo la kuimarika kwa fonimu kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

**/f/ → /p/**

Sifa zao bainifu ambazo zinajitokeza ni zifuatazo;

| /f/ | /p/ |
|---|---|
| +konsonanti | +konsonanti |
| +kikwamizo | +kipasuo |
| +midomo-meno | +midomo |
| -mghuno | -mghuno |

Kutokana na sifa hizi bainifu, /f/ inatofautiana na /p/ katika sifa ya aina na mahali pa kutamkia, ambapo /f/ ni kikwamizo na hutamkwa kwenye midomo meno ilhali /p/ ni kipasuo na hutamkwa kwenye midomo. Kwa hivyo, Sauti /f/ ambayo ni kikwamizo cha midomo meno haipo katika Kikipsigis, hivyo basi inapotokea katika msamiati wa Kiingereza unaoingizwa katika Kikipsigis, hubadilishwa na kuwa /p/ ambayo ni kipasuo cha midomo na hivyo kuimarika kwa mfano;

| **Kiingereza** | → | **Kikipsigis** |
|---|---|---|
| factɔry | → | paktɔri |
| fɔrɛst | → | pɔrɔstɛ |
| prɔfessɔr | → | prɔpɛsa |
| finɛ | → | pain |
| fɔrm | → | pɔmit |
| rɛfɛrɛndum | → | rɛparɛndam |

**/θ/ → /t/**

Sauti /θ/ na /t/ zinabainishwa na sifa bainifu zifuatazo;

| /θ/ | /t/ |
|---|---|
| +konsonanti | +konsonanti |
| +kikwamizo | +kipasuo |

| | |
|---|---|
| +meno | +ufizi |
| -mghuno | -mghuno |

Sauti hizi zinatofautiana katika sifa ya aina ya fonimu na mahali pa kutamkia ambapo, /θ/ ni kikwamizo cha meno ilhali /t/ ni kipasuo cha ufizi. Kwa sababu sauti /θ/ haipo katika Kikipsigis, msamiati mkopo ulio na sauti hii hubadilishwa kuwa /t/ kwa sababu sauti /t/ hukaribia sauti /θ/ kimatamshi kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

| **Kiingereza** | | **Kikipsigis** |
|---|---|---|
| θɛrmɔs | → | tamɔsit |
| Θɛatrɛ | → | tiɛta |

**ii. Vikwamizo (+ghuna)→ vipasuo (-ghuna)**

Kikwamizo kilicho na mghuno kipo katika ngazi ya sita na kinapobadilishwa kuwa kipasuo kisicho na mghuno huwa imeimarika kama ilivyo katika mfano ufuatao:

**/v/ → /p/**

Sauti hizi zina sifa zifuatazo bainifu;

| /v/ | /p/ |
|---|---|
| +konsonanti | +konsonanti |
| +kikwamizo | +kipasuo |
| +midomo meno | +midomo |
| +mghuno | -mghuno |

Sauti /v/ ambayo ni kikwamizo kinachotamkwa wakati mdomo wa chini ukiwa umegusa meno ya juu, hubadilishwa kuwa /p/. Sauti /v/ ni sauti ghuna ilhali /p/ ni sauti isoghuna na kwa kuwa sauti isoghuna ina nguvu matamshi kuliko sauti ghuna, basi /v/ kubadilishwa kuwa /p/ huifanya kuimarika, kama mfano unaofuata unavyoonyesha:

| **Kiingereza** | → | **Kikipsigis** |
|---|---|---|
| rɛvɛrɛnd | → | rɛparɛn |
| drivɛr | → | indɛrɛpayat |
| gɔrvɛnɛr | → | kapana |
| tɛlɛvisiɔn | → | tɛlɛpisiɔn |
| vɛrandah | → | paranda |

**Kudhoofika kwa fonimu konsonanti**

Kudhoofika kwa fonimu ni dhana ambayo wanaisimu hutumia kuelezea ile hali ya fonimu fulani kubadilika kutoka fonimu ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu zaidi na kuwa sauti ambayo hutamkwa kwa kutumia nguvu kidogo kuliko ile ya awali (Mgullu 1999), kama inavyobainika katika mifano ifuatayo:

**i) Vipasuo (-ghuna) → vipasuo ng'ong'o (+ghuna)**

**/t/ → /$^{n}$d/**

Sauti hizi zina sifa bainifu zifuatazo;

| /t/ | /$^{n}$d/ |
|---|---|
| +konsonanti | +konsonanti |
| +kipasuo | +kipasuo ng’ong’o |
| +ufizi | +ufizi |
| -mghuno | +mghuno |

Sauti /t/ ni kipasuo cha ufizi kisicho kuwa na mghuno ilhali /$^{n}$d/ ni kipasuo ng’ong’o cha ufizi kilicho na mghuno. Kwa kuwa utamkaji wa sauti isoghuna /t/ humia nguvu zaidi kuliko utamkaji wa sauti /$^{n}$d/ iliyo na mghuno basi badiliko hili ni la kudhoofika kwa fonimu. Mifano:

| **Kiingereza** | | **Kikipsigis** |
|---|---|---|
| Printɛr | → | Purindait |
| kauntI | → | kɔundi |
| kəntrækt | → | kɔndrakt |
| Kaunter | → | kaɔnda |

**/p/ → /$^{m}$b/**

Sauti hizi zinabainishwa na sifa zifuatazo:

| **/p/** | | **/$^{m}$b/** |
|---|---|---|
| +konsonanti | → | +konsonanti |
| +kipasuo | → | +kipasuo ng’ong’o |
| +midomo | → | +midomo |
| -mghuno | → | +mghuno |

Sauti /p/ ni kipasuo kinachotamkwa kwenye midomo na haina mghuno. /$^{m}$b/ ni sauti ambayo hutamkwa vilevile kwenye midomo na ina mghuno. Katika msamiati asilia wa Kikipsigis, sauti hii hupatikana katika maneno kama vile;

| **Kikipsigis** | **tafsiri** |
|---|---|
| imbarɛt | shamba |
| kambagɛt | uzushi |
| imbɔcɛt | ʃangazi |

Ilibainika kwamba baadhi ya msamiati mkopo kutoka Kiingereza ulio na konsonanti /p/ unapoingizwa katika Kikipsigis, hubadilishwa kuwa /mb/ kama ilivyo katika mifano ifuatayo;

| **Kiingereza** | | **Kikipsigis** |
|---|---|---|
| kəmputer | → | kɔmbyuta |

kʌmpəni → kambunit

Katika mifano hii tunaona kuwa sauti /p/ isiyokuwa na mghuno imebadilishwa kuwa saui /mb/ iliyo na mghuno. Mchakato huu wa kubadilisha /p/ isiyo ghuna kuwa /mb/ iliyo ghuna hufanya sauti hii kudhoofika kwani sauti isoghuna ina nguvu matamshi kuliko sauti ghuna. Mabadiliko haya huenda yanatokea kwa sababu Kikipsigis hakina mfuatano wa silabi /mp/ lakini ina /mb/.

**Udondoshaji wa sauti /h/**

Ingawa Towett (1979) aliorodhesha sauti /h/ kama mojawapo wa konsonanti zilizopo katika Kikipsigis, utafiti wetu ulibainisha kuwa sauti hii haipo katika Kikipsigis. Hii inadhihirika kupitia msamiati unaokopwa ulio na sauti /h/, unapoingizwa katika Kikipsigis, hudondoshwa kwa kuwa haipo katika Kikipsigis. Kwa mfano;

| **Kiingereza** | | **Kikipsigis** |
|---|---|---|
| hɒspitl | → | sipitaliit |
| helikɒpte | → | ɛlicɔptaait |
| hɒlidei | → | ɔlitɛɛi |
| Hall | → | ɔliit |

Katika mifano hii tunaona kwamba sauti /h/ imedondoshwa na kisha nafasi yake kufidiwa kwa kurefushwa kwa irabu mwishoni mwa maneno husika kabla ya kimalizio.

## Utohozi wa konsonanti kutoka Kiswahili

**Kuimarika na kudhoofika kwa konsonanti**

Jinsi ilivyobainika katika mabadiliko ya konsonanti za Kiingereza, kuna kuimarika na kudhoofika vilevile katika utohozi wa konsonanti za Kiswahili.

**Kuimarika kwa konsonanti**

Kuimarika kwa konsonanti ya Kiswahili unapoingizwa katika Kikipsigis hutokea kupita mifano ifuatayo:

i. **Vikwamizo (-ghuna) → vipasuo (-ghuna)**

**/f/ → /p/**

Konsonanti hizi zina sifa bainifu zifuatazo:

| /f/ | /p/ |
|---|---|
| +konsonanti | +konsonanti |
| +kikwamizo | +kipasuo |
| +midomo meno | +midomo |
| -mghuno | -mghuno |

/f/ ni kikwamizwa cha midomo meno, hutamkwa wakati ambapo mdomo wa chini unagusa meno ya juu. Kwa kuwa konsonanti hii haipo katika Kikipsigis, basi ili msamiati mkopo ulio na sauti hii uweze kukubalika katika Kikipsigis hubadilishwa kuwa /p/ ambayo ni kipasuo cha midomo hivyo kuimarika kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

**Kiswahili** **Kikipsigis**

| | | |
|---|---|---|
| elfu | → | eliput |
| safari | → | saparit |
| faida | → | paita |
| bafu | → | papit |

**ii. Vikwamizo (+ghuna) → vipasuo (-ghuna)**

**/v/ → /p/**

Konsonanti hizi zina sifa bainifu zifuatazo;

| /v/ | /p/ |
|---|---|
| +konsonanti | +konsonanti |
| +kikwamizo | +kipasuo |
| +midomo meno | +midomo |
| +mghuno | -mghuno |

Konsonanti /v/ ni kikwamizo kinachotamkwa wakati ambapo mdomo wa chini unagusa meno ya juu. Sauti hii vilevile ina mghuno. Kwa kuwa sauti hii haipo katika Kikipsigis, hubadilishwa kuwa /p/ ambayo ni kipasuo kinachotamkwa midomoni isiyo ghuna na hivyo kuimarika kwa mfano;

| **Kiswahili** | | **Kikipsigis** |
|---|---|---|
| Viazi | → | Piasinik |
| dɛrɛva | → | Indɛrɛpaindɛt |

**Kudhoofika kwa fonimu**

Utafiti huu ulibainisha kuwa hali hii hutokea katika Kikipsigis katika fonimu /k/ , /θ/ na /ʃ/ , kwa mfano:

**i. Vipasuo (-ghuna) → vipasuo (+ghuna)**

**/k/ → /g/**

Sauti hizi zina sifa bainifu zifuatazo;

| /k/ | /g/ |
|---|---|
| +konsonanti | +konsonanti |
| +kipasuo | +kipasuo |
| +kaakaa laini | +kaakaa laini |
| -mghuno | +mghuno |

Sauti /k/ ambayo ni kipasuo cha kaakaa laini kisicho na mghuno hubadilishwa kuwa /g/ ambayo ni kipasuo cha kaakaa laini kilicho na mghuno na hivyo kudhoofika kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

**Kiswahili**

| | | |
|---|---|---|
| As**k**ari | → | asi**gɔ**rindɛt |
| M**k**atɛ | → | ma**g**atiat |
| Hɛ**k**alu | → | ɛ**g**alut |
| ki**kɔ**mbɛ | → | ki**gɔ**mbɛt |
| malai**k**a | → | malai**g**ajat |
| m**kɔ**ra | → | ma**gɔ**rajat |

Tulibainisha katika utafiti huu pia kuwa kuna mabadiliko ya konsonanti yasiyohusisha kuimarika wala kudhoofika kwa fonimu. Mabadiliko haya ni kama yafuatayo:

**i. Vikwamizo (-ghuna) → vikwamizo (-ghuna)**

**/θ/ → /s/**

Sauti hizi zina sifa bainifu zifuatazo;

| / θ/ | /s/ |
|---|---|
| +konsonanti | +konsonanti |
| +kikwamizo | +kikwamizo |
| +meno | +ufizi |
| -mghuno | -mghuno |

Konsonanti /θ/ ni kikwamizo kinachotamkwa kwenye meno ilhali /s/ ni kikwamizo cha ufizi. Kwa sababu Kikipsigis hakina sauti /θ/ maneno yanayosharabiwa yaliyo na sauti hii hubadilishwa kuwa /s/ kwa kuwa sauti hii inakaribiana kimatamshi na /s/ na vilevile ni kikwamizo. Sauti hizi mbili hazina mghuno kwa hivyo zinatumia nguvu sawa katika matamshi na hivyo basi kutoimarika wala kutodhoofika, mifano:

| **Kiswahili** | | **Kikipsigis** |
|---|---|---|
| θumuni | → | sumɔnit |
| θɛlaθini | → | salasini |

**Uchopezi wa Konsonanti**

Katika Kiswahili, asilimia kubwa ya msamiati huwa na silabi wazi, hata hivyo hali ni tofauti katika Kikipsigis kwani hupendelea muundo wa silabi funge. Kwa hivyo, Kikipsigis kinapokopa msamiati kutoka Kiswahili, msamiati huo hutoholewa kwa kuchopekwa konsonanti mwishoni mwa neno ili kuunda silabi funge kama inavyobainika katika mifano ifuatayo;

| **Kiswahili** | | **Kikipsigis** |
|---|---|---|
| Simu | → | simɔi**t** |

Chupa → cupɔit
nganɔ → nganu**k**
maharagwɛ → marakwɛ:**k**
ʃɛhɛrɛkɛa → sjɛrɛgɛa**n**
mɛza → mesait → mɛsɛ**t**
mpira → imbirait → imbirɛ**t**
kanisa → kanisait → kanisɛ**t**

Mifano hii imedhihirisha kwamba Kikipsigis hutohoa msamiati wa Kiswahili ulio na silabi wazi kwa kuongeza konsonanti mwishoni mwa neno husika ili msamiati huo ukubalike katika Kikipsigis. Konsonanti inayochopekwa sana ni /t/ na wakati mwingine /k/ na /n/.

**Udondoshaji wa konsonanti**

Utafiti huu ulibainisha kuwa upo ushahidi wa kutosha kuthibitisha kuwa Kikipsigis hudondosha konsonanti kutoka baadhi ya msamiati mkopo kutoka Kiswahili. Konsonanti zinazodondoshwa ni zile ambazo hazipatikani katika lugha hii, kwa hivyo, zinapopatikana katika msamiati unaokopwa hudondoshwa na nafasi zao kuachwa wazi au kuchukuliwa na konsonanti nyingine inayokaribiana kimatamshi na konsonanti inayodondoshwa.

**Udondoshaji wa konsonanti /h/**

Ingawa Towett (1979) aliorodhesha fonimu /h/ kama mojawapo wa konsonanti za Kikipsigis, data ya utafiti huu umebainisha kwamba fonimu hii haipo katika lugha hii. Hii ni kwa sababu konsonanti hii /h/ hudondoshwa katika msamiati wa Kiswahili unaosharabiwa katika Kikipsigis kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

**Udondoshaji wa /h/ mwanzoni mwa msamiati**

| **Kiswahili** | | **Kikipsigis** |
|---|---|---|
| hɛsabu | → | ɛsapuuk |
| hɛkalu | → | ɛgaluut |
| harusi | → | arusiit |

Mifano hii inaonyesha kwamba, /h/ inapotokea mwanazoni mwa neno hudondolewa na nafasi yake kuachwa wazi kwa sababu sauti hii haipo katika Kikipsigis. Hata hivyo tunaona kwamba katika maneno mengine, udondoshaji wa /h/ mwanzoni mwa msamiati hufidiwa kwa kurefushwa kwa irabu inayotokea mwishoni mwa neno hilo kama ilivyo katika [hekalu → ekaluut], [hoteli → oteliit].

**Udondoshaji wa /h/ katikati ya msamiati**

Katika udondoshaji wa /h/ katikati mwa neno tulibainisha kwamba sauti hii hudondoshwa na nafasi yake ama kuachwa wazi au kuundwa kwa kiyeyusho [j] au pia /h/ kudondoshwa pamoja na irabu inayofuata mathalani:

Udondoshaji wa /h/ na nafasi yake kuachwa wazi hubainika katika;

mhɔgɔ → mɔgɔ

Udondoshaji wa /h/ na nafasi yake kuchukuliwa na kiyeyusho [j];

bahaʃa → pasjait

mʃahara → musyara

Shɛhɛrɛkɛa → sjɛrɛgɛan

Udondoshaji wa /h/ pamoja na irabu katikati ya neno;

sahani → saniit

bahari → pariit

ruhusa → rusa

maharagwɛ → marakwɛ:k

Katika mifano hii, /h/ inapodondoshwa, irabu mbili zitafuatana na hivyo kuibua muundo usioleta maana katika Kikipsigis kwa mfano;

sahani → saaniit

bahari → paariit

Kwa hivyo,, Kikipsigis haina budi kuondoa irabu moja kati ya hizo mbili ili kunda msamiati unaokubalika na ulio na maana katika Kikipsigis mathalani:

sa**ha**ni → s**aa**nit → s**a**niit

ba**ha**ri → p**aa**rit → p**a**riit

Mifano hii hivyo basi imedhihirisha kwa uwazi kuwa sauti /h/ haipo katika Kikipsigis na hii ndio sababu sauti hii hudondolewa katika msamiati mkopo wa Kiswahili unapoingizwa katika lugha hii.

**Sababu za kiisimujamii zinazochangia ukopaji wa msamiati katika Kikipsigis**

Myers-Scotton (2002) anaeleza kuwa mitagusano baina ya lugha husababisha athari mbalimbali katika lugha hizo. Matokeo ya mtagusano wa lugha ni pamoja na ukopaji wa msamiati, ujozi lugha na uundaji wa Pijini na Krioli. Anazidi kufafanua kwamba sifa iliyo wazi ya kiisimujamii kuhusu ukopaji wa msamiati ni kuwa katika lugha nyingi ulimwenguni, ukopaji huelekea katika upande mmoja ambapo wasemaji wa lugha iliyo na hadhi ya chini huchukua msamiati/maneno kutoka lugha iliyo na hadhi ya juu. Nchini Kenya, kwa mfano, lugha za Kiswahili na Kiingereza zinachukuliwa kuwa lugha zilizo na hadhi ya juu kwa sababu Kiingereza ni lugha rasmi na hutumika katika mawasiliano ya kimataifa, Kiswahili kwa upande wake ni lugha ya taifa na vilevile ni lugha rasmi.

Utafiti huu ulibainisha aina mbili za ukopaji: ukopaji wa msamiati wa kiutamaduni na ukopaji wa msamiati wa kimtindo. Katika ukopaji wa kiutamaduni, msamiati unaokopwa ni ule unaorejelea dhana geni ambayo haijakuwepo katika utamaduni wa lugha inayokopa. Kwa upande mwingine, ukopaji wa kimtindo hurejelea ukopaji wa msamiati wa kigeni wakati ambapo kuna

kisawe au msamiati asilia unaorejelea dhana hiyo hiyo. Ukopaji wa kiutamaduni umedhihirika katika Kikipsigis ambapo lugha hii imekopa msamiati kutoka Kiswahili na Kiingereza ili kurejelea dhana geni katika nyanja mbalimbali kama vile uwanja wa sayansi na teknolojia, elimu, uchumi, mavazi, miundo misingi na nyanja nyinginezo. Kwa mfano; simoit (simu), stima (sitimet), kitabu (kitapuut) jinsi inavyodhihirika ifuatavyo:

| **(a) Kiswahili** | | **Kikipsigis** | |
|---|---|---|---|
| chuma | → | chumoiyot | |
| risasi | → | risasyat | |
| bunduki | → | pundugit | |
| **(b) Kiingereza** | | **Kikipsigis** | **Kiswahili** |
| factory | → | paktori | kiwanda |
| machine | → | mosyinit | mashine |
| nursery | → | nasaret | chekechea |

Dhana hizi hazikuwepo katika utamaduni wa Wakipsigis. Kwa hivyo, Kikipsigis kimekopa na kutohoa kutoka lugha ya Kiswahili na Kiingereza ili kutumika kuzirejelea dhana hizi geni. Ukopaji wa kimtindo huhusisha ukopaji wa msamiati kutoka lugha bebwa ili kuchukua nafasi ya kisawe chake cha kiasili (Myers-Scotton (2002:41). Hali hii husababishwa na ubadilishaji msimbo. Tofauti na ukopaji wa kiutamaduni ambapo msamiati hukopwa ghafla ili kurejelea dhana geni na kujaza pengo la ukosefu wa msamiati, katika ukopaji huu, msamiati mkopo huingia katika lugha asilia kiutaratibu. Uchanganuzi ulibainisha kuwa, kutokana na elimu ya kimsingi, wanaujozi lugha wa Kikipsigis, Kiswahili na Kiingereza wameingiza misamiati ya lugha hizi bebwa katika Kikipsigis hata ingawa kuna msamiati asilia jinsi inavyobainika katika nyanja mbalimbali kama vile uwanja wa vifaa vya kinyumbani, uongozi, mavazi, dini, miongoni mwa nyanja nyinginezo. Utafiti ulibainisha kwa mfano kwamba Kikipsigis hukopa msamiati wa kigeni ili kurejelea vifaa vya kinyumbani ilhali kuna msamiati asilia wa Kikipsigis kama ilivyo katika mifano ifuatayo:

| **(a)** | **Kiswahili** | **msamiati mkopo** | **msamiati asilia** |
|---|---|---|---|
| | mlango | mlangoit | kurget |
| | kitanda | kitandet | kitogit |
| | kifuniko | kifuniget | kereywot |
| **(b)** | **Kiingereza** | **msamiato mkopo** | **msamiati asilia** |
| | stool | stulit | ng’echeret |
| | brush | purasit | kipsitet |

Katika mifano hii, ilibainika kwamba ingawa Kikipsigis kina msamiati wa kiasili wa kurejelea dhana hizi, wanatumia msamiati uliotoholewa kutoka Kiswahili na Kiingereza. Ingawa wanaujozi lugha ndio huingiza misamiati hii mikopo katika Kikipsigis, baada ya matumizi ya muda, inakubalika katika jumuiya lugha ya Wakipsigis na hivyo hata wale ambao hawana elimu wanaweza kuitumia.

**Hitimisho**

Kimsingi, uchanganuzi wa mabadiliko ya kimofofonemiki katika msamiati mkopo wa Kikipsigis kutoka Kiingereza na Kiswahili umebainisha kuwa irabu katika msamiati wa Kiingereza hutoholewa kupitia ufupishaji wa irabu ndefu, usahilishaji wa irabu unganifu, uyeyushaji na muungano wa irabu. Katika irabu za Kiswahili, utohozi hufanyika kupitia uchopezi wa irabu, tangamano la irabu/kuafikiana kwa irabu, mvutano wa irabu na udondoshaji wa irabu. Kwa upande mwingine, michakato inayotumika katika utohozi wa konsonanti za Kiingereza na Kiswahili zinafanana. Michakato hiyo ni pamoja na kuimarika kwa kosnonanti, kudhoofika kwa konsonanti, uchopezi wa konsonanti na vilevile udondoshaji wa konsonanti. Usilabishaji hufanyika kupitia uchopezi wa irabu mwanzoni mwa msamiati ulio na mfuatano wa konsonanti mbili. Usilabishaji pia hufanyika kupitia uchopezi wa konsonanti mwishoni mwa msamiati ulio na muundo wa silabi wazi kwa sababu Kikipsigis hupendelea muundo wa silabi funge.

**Marejeleo**


Asher, R.E. & Simpson, J.M.Y (1994). *The Encyclopedia of Language and Linguistics.* Vols. 1 & 4. Oxford: Pergamon Press.

Aswani, F.O. B. (1995). *Fonolojia ya Silabi ya Kiswahili Sanifu na ya Kimarama*: Uchunguzi Linganishi. *Tasnifu ya Uzamili* Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).

Bright, W (1997). *Social Factors in Language Change*. Katika Coulmas, F (mhariri), *The Handbook of Sociolingustics.* Cambridge: Blackwell Publishers Ltd.

Habwe,J. & Karanja P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Iribemwangi, P.I. & Mukhwana A. (2011). *Isimujamii.* Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Kadurenge, K. (1995). *Mabadiliko ya Kifonolojia ya msamiati Uliosharabiwa kutoka Kiswahili hadi Kimaragoli.* Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Moi. (Haijachapishwa).

LaCharite, D. & Paradis, C. (2000). Phonological evidence for Bilingualism of Borrowers. Katika: J. Jensen & G. Van Herk (whr.) *Proceedings of the 2000 Annual Conference of ‘The Canadian Linguistics Association*’ Ottawa: Cahiers Linguistiques d’Ottawa.

McMahon, A. (1994). *Understanding Language Change*. Cambridge: Cambridge University Press.

Mgullu, S.R. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Longman Publishers. Nairobi.

Muysken, P. (1995). Code-switching and Grammatical Theory. Katika: Milroy & P. Muysken (Whr) *One Speaker Two Languages*. Cambridge: Cambridge University press.

Myers-Scotton, C. (2002). *Contact Linguistics*: Bilingual Encounters and Grammatical Outcomes. New York, Oxford University Press.

———— (1997*). Duelling languages: Grammatical Structure in Codeswitching* (with a new Afterword). Oxford: Clarendon Press.

————(1993). *Social Motivation for Codeswitching*: Evidence from Africa. Oxford: Clarendon Press

———— (1992). Codeswitching as a Mechanism in Deep Borrowing, Language Shift, and Language Death. Katika: M. Brenzinger (Mhr.), *Language Death, Factual and Theoretical Explorations with Special Reference to East Africa,* 31-58. Berlin: Mouton de Gruyter.

Roach, P. (2000). *English Phonetics and Phonology: A Practical Course*. Cambridge University Press.

Sambu, K. (2007). *The Kalenjiin People’s Egypt Origin Legend Revisited: Was Isis Asiis:* Longhorn Publishers.

Sang, H.K. & Jerono, P. (2012). The Phonology of Loanwords in three Kalenjin Dialects. Katika: Ogechi, N.O, Jane A. & Iribemwangi, P. (Whr). *The Harmonization and Standardization of Kenyan Languages*. Cape Town: CASAS.

Seroney, K. (2009). *Samburtaab Ng’aleekaab Keleenchin: Kalenjin Dictionary*. Mvule Africa Publishers.

Towett, T. (1979). *A Study of Kalenjin Linguistics.* Kenya Literature Bureau. Nairobi|.

TUKI (1990). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam. Oxford University press.

Whitefield, L.H. (1970). *Language: An Introduction to Social. Madison*: University of Wisconsin Press.

Yule, G. (2006). *The Study of Language.* Cambridge: Cambridge University Press.